

SEHEMU YA 1
LUGHA NA ELIMU

BAKITA NA LUGHA YA KUFUNDISHIA

Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)

Ikisiri

Makala haya yanatoa maelezo mafupi ya matukio muhimu kuhusu suala la kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia sekondari na vyuo katika kipindi baina ya mwaka 1967 mpaka 2000. Makala yanaeleza dhima na shughuli za BAKITA na asasi nyingine za ukuzaji wa Kiswahili. Halikadhalika, makala yanaeleza mabadiliko ambayo yamekuwa yakitokea katika mtazamo wa serikali kuhusu Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia. Hadi kufikia mwaka 1971, serikali ilitilia mkazo azma hiyo itimizwe. Lakini baada ya mwaka huo mkazo ulianza kupungua. Hadi leo serikali imekuwa ikikataa hata mapendekezo yatokanayo na tafiti ilizozigharamia. Mapendekezo ya utafiti wa Mlama na Manneru (1980) uliogharamiwa na BAKITA, na mapendekezo ya utafiti wa Tume ya Kuchunguza Mfumo wa Elimu (1982) uliogharamiwa na serikali, ni baadhi tu ya tafiti kama hizo. Mbali na tabia hiyo ya ugeugeu wa serikali, makala inaeleza hatua mbalimbali ambazo BAKITA imechukua kukiwezesha Kiswahili kufundishia sekondari na vyuo miongoni mwake zikiwemo kuratibu shughuli ya kutafsiri vitabu vya kiada kwa masomo mbalimbali ya sekondari, kuandaa kongamano la kimataifa mnamo mwaka 1991 ambalo limesaidia kuhuisha tena matumizi ya kuthamini Kiswahili, kuanzishwa kwa siku ya Kiswahili tangu 1995 na uundaji wa kamati maalum mwaka 2000 ili kuchochea upya uwezo wa Kiswahili kupanuka katika matumizi hasa katika kufundishia sekondari na vyuo. Yote haya yanafanyika katika hali ngumu kifedha, ambayo imekuwa ikiikabili BAKITA kwa kipindi kirefu sasa.

1.0 Utangulizi

Mara baada ya uhuru, Kiswahili kilitangazwa kuwa lugha ya Taifa, na Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Tanganyika Mwalimu Julius K. Nyerere alilikutubia Bunge kwa Kiswahili mwaka 1962. Huu ulikuwa ushahidi wa kutosha wa kuipa hadhi Lugha ya Kiswahili iliyotumika katika harakati za kuikomboa na kuishikamanisha nchi yenye makabila zaidi ya 120. Baada ya uhuru, taifa lilijiwekea malengo yake na maslahi ya utamaduni wa taifa yakapewa kipaumbele kwa kuanzishwa asasi mbalimbali za utamaduni ikiwemo Wizara ya Utamaduni mwaka 1962, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili mwaka 1964, Shirika la Uchapishaji Vitabu ya Tanzania (THP) mwaka 1966, Baraza la Kiswahili la Taifa mwaka 1967 na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1970.

Sheria nambari 27 ya mwezi Agosti mwaka 1967 inalipa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) jukumu la kusimamia maendeleo ya Kiswahili katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. BAKITA ndiye mratibu mkuu wa shughuli zote za Kiswahili nchini. Miongoni mwa mambo muhimu ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili ni kuhakikisha kwamba lugha hii inatumiwa ipasavyo katika sekta zote za maisha ya Mtanzania ikiwemo elimu.

2.0 Sera ya Serikali Kuhusu Lugha ya Kufundishia

Tukio muhimu kuliko yote yalitokea mwaka 1967 si kuundwa kwa Baraza la Kiswahili la Taifa bali ni kupitishwa kwa Azimio la Arusha ambalo lilifanua Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea kuundwa kwa BAKITA. Kuratibu shughuli za lugha ni matokeo ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Ilitamkwa kwamba Kiswahili kitumike kufundishia elimu yote ya msingi. Kabla ya hapo ni madarasa manne tu ya mwanzo ya shule za msingi ndiyo yaliyotumia Kiswahili; Kiingereza kilitumiwa kwa kufundishia madarasa yote ya juu. Uamuzi huu wa busara na wa kizalendo unaojali maslahi ya wengi ulifuatiwa na uamuzi mwingine muhimu wa kutumia Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika vyuo vya ualimu ambavyo huwaandaa walimu wa shule za msingi watakaohudumia shule hizo chini ya mpango wa Elimu ya Msingi kwa Wote mapema mwaka 1970 (Msanjila 1990:307).

Ili kupata uwiano mzuri wa lugha ya kufundishia elimu nchini Tanzania, ilitarajiwa kwamba Kiswahili kingefanywa lugha ya kufundishia katika shule za sekondari na vyuo vingine vya juu. Kama ilivyobainishwa na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 1969/70 – 1973/74 kwamba:

Tutaelekea katika utaratibu wa elimu ambao masomo yanafundishwa kwa lugha ya Kiswahili kutoka shule za msingi, ambapo masomo katika shule za sekondari na zaidi hufundishwa kwa Kiingereza. Hata hivyo mabadiliko haya yanaleta matatizo ya elimu, na pia hatari kubwa katika maisha ya watu. Tofauti kati ya wale waliojifundishia Kiswahili katika Shule ya Sekondari itaunda na kudumisha tabaka za lugha na kuifanya elimu ya juu ya kigeni isiyohusiana na matatizo ya umma. Hali hii haitaweza kuvumiliwa kama itadumu. Hasa jinsi Serikali inavyoendelea kutumia Kiswahili katika kazi zake; itazidi kuwa haifai kutoa mafunzo katika Shule za Sekondari na shule za juu zaidi kwa lugha ya Kiingereza ... (Mlama na Mattered, 1980:5).

Mwelekeo huu wa Serikali wa kutia moyo uliungwa mkono kwa vitendo na taasisi za serikali kwa kubuni mipango itakayohakikisha kwamba Kiswahili kinachukua nafasi ya Kiingereza kufundishia elimu ya sekondari na ya juu hatua kwa hatua.

Mwaka 1970, tarehe 5-9 Juni, Baraza la Kiswahili la Taifa lilitisha semina ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, iliyoshirikisha asasi zote zinazokuza Kiswahili Tanzania Bara na Visiwani. Aidha ilipata heshima ya kutiwa shime na viongozi wa ngazi za juu serikalini. Katika hotuba ya kumkaribisha mgeni rasmi, ambaye alikuwa ni Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Rashid M. Kawawa ili afungue semina hiyo, Mwenyekiti wa BAKITA, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, alisema:

Madhumuni ya mkusanyiko huu ni kuzungumza, kupeana rai, kulinganisha jitihada zetu, kujadili matatizo na kutafuta njia za kukuza, kustawisha na kueneza Kiswahili katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania... Vile vile tunafahamu kuwa Lugha ya Taifa lolote inastahiki kutukuzwa na kuheshimiwa na watu wake.... Tumekualika ili uendelee kutupa mawaidha yako ya busara na utupe wasia utakaokuwa mwangaza kwetu wa kumulikia njia yetu itakayotufikisha kwenye lengo letu - nalo

ni mapinduzi ya kukitawalisha Kiswahili ili kiweze kutumika, kwa kutosheleza, katika mahitajio ya aina zote za maisha ya Watanzania....

Katika ufunguzi wa Semina hiyo, Mheshimiwa Rashid M. Kawawa aliwatia moyo, ari na kuwapa changamoto wakuzaji Kiswahili kwa kueleza kiini cha kasumba ya kujali lugha ya kigeni, “Katika miaka mingi ya kutawaliwa, kuonewa na kupuuzwa, jambo ambalo mkoloni alifanikiwa sana kufanya ni kutudhalilisha utu wetu, tukapata unyonge wa moyo, unyonge uliotufanya tuthamini sana mabwana, lakini tusijithamini sisi wenyewe... Hivyo ndivyo asili ya kupuuzwa sana kwa lugha yetu ya Kiswahili. Sisi wenyewe tukawa tunaona fahari sana kusema Kiarabu au Kiingereza, japo cha kubabaisha, na Kiswahili tukakionea haya...”

Huu ni uthibitisho mwingine wa mwamko na kuhamasika kwa viongozi wetu katika kuunga mkono maamuzi ya serikali na vyombo vyake vinavyokuza lugha. Ni vema ifahamike kwamba taifa halikamiliki bila ya kuwa na lugha yake inayotukuka miyoni mwa wananchi wenyewe. Kuundwa kwa BAKITA kwa mujibu wa sheria, ni mfano mwingine wa juhudi za serikali kuikuza na kuitukuza lugha ya Kiswahili, ambayo imedhalilika kwa miaka mingi.

3.0 Maandalizi ya Istilahi kwa Shule za Sekondari

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, Baraza la Kiswahili la Taifa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na asasi nyingine za kukuza Kiswahili, ziliitikia wito wa semina ya Juni mwaka 1970 kwa kuandaa istilahi ambazo zingesaidia katika uandikaji wa vitabu vya kufundishia viwango mbalimbali vya elimu nchini Tanzania. BAKITA iliratibu zoezi zima kwa kuitisha warsha za usanifishaji wa istilahi zilizochapishwa katika vijitabu vya marejeo katika mfululizo wa *Tafsiri Sanifu*, (Toleo la Pili 1976, Toleo la Tatu 1978, Toleo la Nne 1980, Toleo la tano 1985), *Kamusi ya Agronomia na Ufugaji* (1989), *Kamusi ya Istilahi za Sayansi na Tekinolojia 1992*.

Sambamba na machapisho hayo, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilichapisha *Kamusi Sanifu ya Isimu ya Lugha* (1990) na *Kamusi Sanifu ya Biolojia, Fizikia na Kemia* (1990) na IPI ilichapisha *Primary Technical Dictionary* (1987). Pamoja na jitihada zote hizo za kuitisha warsha za usanifishaji wa istilahi na kuchapisha marejeo mbalimbali, serikali haikuchukua hatua yoyote ya kubadili mwelekeo wake kuhusu lugha ya kufundishia. Badala yake, Kiingereza kiliendelea kujichimbia katika kufundishia elimu ya sekondari na elimu ya juu.

4.0 Utafiti wa Haja ya Kutumia Kiswahili Kufundishia Elimu ya Juu (Mlana na Materu 1978)

Ingawa shughuli za maandalizi ya istilahi zilionyesha kugonga ukuta kutokana na Kiingereza kuendelea kutumika kufundishia, BAKITA kwa upande wake halikuvunjika moyo wala kukatishwa tamaa na tabia ya serikali ya kutothamini maamuzi yake kuhusiana na Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari na ya juu. Mwaka

1977, lilidhamini utafiti uliofanywa na P.O. Mlama na M.L. Materu ambao wakati huo walikuwa wajumbe wa Baraza hilo. Utafiti wao ulihusu hali ya matumizi ya lugha katika kufundishia na jinsi lugha ya kufundishia inavyoathiri elimu na jamii nchini Tanzania. Watafiti hao walitembelea shule za msingi sita, shule za sekondari 16 na vyuo vya Elimu vitatu katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Dodoma na Mbeya ambako walizungumza na walimu na wanafunzi. Aidha waliwapa walimu na wanafunzi maswali ya kuandika na hata kuhudhuria vipindi darasani (vya Kiingereza katika shule za msingi, vya masomo yanayofundishwa kwa Kiingereza katika shule za Sekondari) na kuzungumza na maofisa elimu na maofisa utamaduni wa mikoani na wilayani. Matokeo ya utafiti huo yalidhihirisha kwamba kulikuwa na matatizo katika kufundisha kwa Kiingereza na pia katika ufundishaji wa somo lenyewe la Kiingereza. Wanafunzi wa shule za msingi ambao hufundishwa kwa Kiswahili na wanapoingia Sekondari wanakabiliwa na badiliko la ghafla la mawasiliano. Ujuzi wa Kiingereza walioupata ni mdogo kwa sababu walimu waliowafundisha nao hawana msingi madhubuti wa lugha ya Kiingereza na mbinu za kufundishia. Kwa kuwa lengo la serikali ni kupata walimu wengi kwa haraka ili kukidhi mahitaji ya elimu ya msingi kwa wote, wamepewa mafunzo ya juujuu ya kufundishia masomo mengi kwa wakati mmoja, k.v. Kiswahili, Kiingereza, Hesabu, Siasa, Sayansi, Jiografia, Historia, Sayansi Kimu, Sanaa na Ufundi, Muziki na Elimu ya Watu Wazima. Aidha wanatakiwa washiriki katika miradi na hivyo kukosa msingi wa mafunzo ya stadi za kufundishia na kujifunzia lugha.

Vilevile utafiti huo ulichunguza utaratibu wa utahini na kugundua kwamba maswali ya kuchagua yanayotolewa mwisho wa mafunzo ya elimu ya msingi hayawapi wanafunzi ujuzi na stadi za lugha kwa sababu wanaandaliwa kuchagua majibu na si kujadili.

Kwa upande wa sekondari, utafiti uligundua kwamba ufundishaji wa somo la Kiingereza haufungamani na matumizi ya stadi nyingine pamoja na miundo, mitindo na msamiati. Hali hiyo inawakosesha wanafunzi uzoefu wa kutosha katika kusema na kujieleza kwa lugha ya Kiingereza.

Kutokana na hali hiyo watafiti walipendekeza kuwa hatua zichukuliwe ili kunusuru elimu Tanzania. BAKITA ilijadili utafiti uo na matokeo yake na kuyawasilisha Wizara ya Elimu kwa nia na madhumuni ya kuhimiza Chama na Serikali kuthamini maamuzi yake na kukubali kuweka mpango madhubuti wa utekelezaji wa hatua kwa hatua kama ilivyofanya mwaka 1969 kwa kutoa agizo lifuatalo kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Taifa upande wa sekondari ingawa halikutekelezwa:

Sasa wakati umefika kuanzisha matumizi ya Kiswahili kuwa ndio lugha ya kufundishia katika shule zetu zote za Sekondari. Naamini kabisa inawezekana kuanza kutumia Kiswahili kufundishia masomo yafuatayo kwenye madarasa ya tisa na kumi mwaka 1970/71.

1. Historia 1971
2. Jiografia 1971
3. Elimu ya Siasa na Elimu ya leo 1969/70
4. Hesabu 1971
5. Elimu ya Viumbe 1971
6. Kilimo 1971
7. Maarifa ya Nyumbani 1973

Kusema kweli kama maamuzi na maagizo yangefuatiliwa na kutekelezwa, matatizo ya lugha ya kufundishia yangukuwa leo hii ni historia tu.

5.0 Tume ya Kuchunguza Mfumo wa Elimu

Kinyume na matarajio ya Watanzania wengi na hasa wakuzaji wa lugha nchini Tanzania, mwezi Novemba mwaka 1980 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu J.K. Nyerere aliteua Tume ya Kuchunguza Mfumo wa Elimu Tanzania na kutoa mapendekezo kuhusiana na marekebisho yanayohitajika kufanywa. Tume hiyo iliyokuwa na uwakilishi wa wataalamu anuai waliobobea katika masuala ya Elimu, Siasa, Isimu ya Lugha na wengineo, ilikusanya maoni ya wananchi na kutembelea nchi za nje zinazotumia lugha zao kufundishia ili kujikusanyia uzoefu wa nchi hizo na kuwa na msingi madhubuti wa kufanyia uamuzi.

Tume ilijaribu kutambua dosari zilizopo na kuzingatia malalamiko na madai ya wananchi kuhusu elimu katika miaka ya karibuni. Maoni yalikusanywa kutoka kwa wataalamu wa sekta zote za maendeleo ya taifa, walimu, wanafunzi, wazazi, wakulima na wafanyakazi viwandani, mashirika, n.k.

Baada ya kuzingatia hayo, ilikamilisha uchambuzi na kutoa ripoti kwa Rais mwaka 1982. Kwa upande wa lugha ya kufundishia ilitoa pendekezo lifuatalo:

Ili taifa liweze kukuza na kuendeleza Utamaduni wake na kurahisisha ufahamu wa wananchi wengi wa masomo katika ngazi za elimu baada ya elimu ya msingi bila kipingamizi cha Lugha za Kigeni, inapendekeza kwamba, Wizara ya Elimu kwa Kutumia vyombo vyake – Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, Vyuho Vikuu na ushirikiano na Baraza la Kiswahili la Taifa, ifanye mipango thabiti ya kuziwezesha shule na vyuo vyote nchini kufundisha masomo yote kwa kutumia Kiswahili kuanzia kidato cha kwanza (cha mfumo wa sasa wa Elimu ya Sekondari) ifikapo mwezi Januari 1985 na Chuo Kikuu kuanzia mwaka 1992. (uk.209).

Kusema kweli hili lilikuwa pendekezo la kishujaa na kizalendo. Serikali, kupitia Wizara ya Elimu, ilitoa tamko mwaka 1984 juu ya Mfumo wa Elimu Tanzania na maamuzi ya chama na serikali kuhusu Ripoti ya Tume ya Rais ya Elimu ya 1982. Tamko hilo lilisisitiza kuwa Kiingereza kiimarishwe kama lugha ya kufundishia elimu ya juu. Huu ni uthibitisho mwingine wa wazi wa Serikali kutozingatia ukweli halisi hata kwa jambo ambalo imeligharamia yenyewe.

6.0 Taasisi ya Elimu Kusita Kukuza Istilahi

Pamoja na majukumu ya kukuza mfumo wa elimu ambayo taasisi hii imepewa na serikali, imesita kuendeleza istilahi za masomo mbalimbali kama ilivyokuwa kuanzia miaka ya 1970 na katikati ya miaka ya 1980 kutokana na msimamo wa serikali ambao tumeshaeleza. Hii imewafadhaisha sana walimu katika shule za sekondari na vyuo ambao hukabiliwa na matatizo ya mawasiliano kama ambavyo tafiti nyingine mbalimbali

zilizvyodhihirisha. Kwa mfano Ripoti ya Utafiti wa Criper na Dodd (1984) uliofadhiwa na Uingereza kupitia Shirika la British Overseas Development Administration (ODA) uliochunguza ujuzi wa lugha ya Kiingereza katika mfumo wa elimu nchini, ilidhihirisha kwamba Kiingereza si njia ya ufanisi katika kutolea elimu katika shule za sekondari. Matokeo haya yalizidi kuishawishi Uingereza kuanzisha Mradi wa Kukuza Kiingereza nchini katika shule za sekondari uliojulikana kama English Language Teaching Support Project – ELTSP. Mradi huo ulioanza mwaka 1986 na uligharimia usambazaji wa vitabu vya kujisomea katika shule za sekondari na kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa walimu wa somo la Kiingereza. Hali kadhalika utafiti wa Campbell na Qorro (1986), uliozingatia uwezo wa kusoma na kuelewa vitabu vya Kiingereza miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari ulidhihirisha kwamba uwezo wa wanafunzi wa sekondari wa kusoma na kuelewa vitabu vya kiada ni mdogo mno kiasi kwamba kati ya asilimia 94% na 95% ya wanafunzi hawawezi kusoma na kuelewa vitabu vinavyotumika shuleni (Qorro, kuhusu Lugha ya kufundishia Rai 5-11/12/96).

Ugeugeu wa serikali yetu ya Tanzania haushangazi kwani tabaka tawala bado lina mtazamo hasi wa kukiona Kiingereza kuwa ni bora; hawa hudhani bila Kiingereza Tanzania haiwezi kuendelea. Hoja hii inaibua maswali mbalimbali kwa watafiti kama Mosha (1990) aliyedhihirisha kwamba pamoja na kukifanya Kiingereza kiweze kupatikana kwa kila mtu mwenye uwezo, hakuna Watanzania wengi wanaokimudu. Ni asilimia 3.3% ya wanaomaliza elimu ya msingi ndio wanaochaguliwa kuingia shule za sekondari. Je, ina maana kwamba Tanzania inalazimika kutumia fedha nyingi kwa manufaa ya lugha ya kigeni kwa ajili ya wachache?

7.0 Juhudi za Wataalamu Binafsi

Kusema kweli hali hiyo ya ugeugeu wa serikali kutokubaliana na hata kile ilichokigundua yenyewe kwa njia ya utafiti kuhusu uwezo wa Kiswahili ni uthibitisho wa kutokuwa na nia thabiti kuhusu Kiswahili kufundishia Elimu ya Juu. Hata hivyo wataalamu binafsi mbalimbali katika fani ya sayansi wamekuwa tangu miaka ya 1970 na 1980 wakifuatilia kwa makini maendeleo ya istilahi za Kiswahili katika fani ya sayansi na fani nyingine. Hii inathibitishwa na orodha ya vitabu mbalimbali vya stadi za sayansi na tekinolojia vilivyotungwa na wataalamu na taasisi mbalimbali nchini. Wote hao wamekuwa wakishauriana na BAKITA na TUKI kuhusu istilahi za fani zao. Juhudi kama hizi zinafaa kuigwa na daima zitabaki katika kumbukumbu za maendeleo ya Kiswahili nchini Tanzania.

- | | |
|------------------|--|
| Geranija, P. | (1982), <i>Elimu ya Sayansi kwa Shule za Msingi</i> , African Publishers, Dar es Salaam. |
| Irira, S.D. | (1979), <i>Kemia ya Mwanzo</i> , TPH, Dar es Salaam. |
| Irira, S.D. | (1980), <i>Fizikia ya Mwanzo</i> , TPH, Dar es Salaam. |
| Kiputiputi, O.M. | (1983), <i>Misingi ya Fotografia</i> , TPH, Dar es Salaam. |
| Kyauka, P.S. | (1980), <i>Misingi ya Sayansi</i> TPH, Dar es Salaam. |
| Lawuo, Z.A. | (1982), <i>Sayansi Longman</i> , Tanzania, Dar es Salaam. |
| Madala, A.N. | (1976), <i>Dunia ya Mashine</i> , TPH, Dar es Salaam. |
| Maige, A.A. | (1981), <i>Misingi ya Umeme na Sumaku</i> , Longman, Tanzania, |

- Dar es Salaam.
- Marto, J.M. (1977), *Uchongaji na Ukerezaji Vyuma*, Dar es Salaam.
- Neema, A.F. (1981), *Sayansi kwa Shule za Msingi*, Black Star Agencies Dar es Salaam.
- Mujemula, F.K. (1977), *Jinsi ya Kufundisha Maksai na Punda Kilimo na Uchukuzi*, TPH Dar es Salaam.
- Nkondokaya, J.R. (1980), *Jinsi Gari Linavyofanyakazi*, TPH, Dar es Salaam.
- Nkondokaya, J.R. (1983), *Injini ya Diseli*, TPH, Dar es Salaam
- Nkondokaya, J.R. (1983), *Matatizo ya Gari na Marekebisho Yake*, TPH Dar es Salaam
- Saka, A.O.J. (1983), *Teknolojia Katika Karakana*, TPH, Dar es Salaam.
- Chuwa, A.R. (WP.5), *Kiongozi cha Kompyuta ()* TUKI.
- Saffari A.J. (2000), *Mashitaka ya Jinai na Utetezi*, Dar es Salaam, UWAVITA.
- Kiputiputi, O.M. (1984), “Fizikia Sehemu ya I” – Umakanika, DUP, Dar es Salaam.
- Kiputiputi, O.M. “Fizikia Sehemu ya II – Umeme na Usumaku” (utachapishwa hivi karibuni).
- Irira, S.D. (1995), *Kamusi Awali ya Sayansi na Teknolojia*, Ben and Company, Dar es Salaam.
- Mlacha, S.A.K. (1999), *Kamusi ya Sheria*, TUKI, Dar es Salaam.
- Mwansoko, H.J.M. & Tumbo Masabo, Z.N. (1998), *Istilahi za Ufundi Magari*, Tuki Dar es Salaam.
- Mwansoko, H.J.M., Nshubemuki, L. Mugasha, A.G. (1999), *Istilahi za Elimu Misitua*, KAD Associates – Publishers.

8.0 Warsha ya Kimataifa

“Dhima ya Lugha katika Elimu ya Msingi, Mashariki mwa Afrika: Msisitizo kwenye Lugha ya Kiswahili” (The Role of Language in Primary Education in Eastern Africa: Special Reference to Kiswahili) ni warsha iliyofanyika tarehe 2-11 Septemba, 1991 ambapo BAKITA ilikuwa ni mratibu. Warsha hii ilifadhiliwa na Deutsche Stiftung fur Internationale Entwicklung kupitia Goethe Institut ambayo ni Taasisi ya Utamaduni ya Kijerumani. Wazo la kuwa na warsha hii liliandaliwa kwa pamoja baina ya BAKITA na Chama cha Kiswahili cha Kenya, ili kujadili na kuweka mikakati kuhusu lugha ya Kiswahili katika Elimu ya Msingi yaani umuhimu wake katika matumizi na mbinu za kufundisha ili kumuwezesha mwanafunzi kupata, kuyaelewa na kuchanganua maarifa afundishwayo.

Mada zilizowasilishwa zilihusu ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika elimu ya msingi, masuala ya vitabu, walimu na umilisi wa Kiswahili kwa watoto na walimu hasa ikizingatiwa kwamba Kiswahili si lugha-mama kwa watoto na walimu wengi lakini ni muhimu sana kama lugha ya taifa katika Tanzania na Kenya.

Warsha ilisisitiza kuwapa mwamko wa kutambua kwamba suala la lugha katika taifa ni mhimili wa kuamua mafanikio au kushidwa kwa elimu ya msingi nchini. Suala la lugha ya kufundishia halina budi lipewe umuhimu wa pekee na kwa kuwa Kiswahili ni lugha

inayotumika katika kufundishia katika shule za msingi, hasa nchini Tanzania, hapana budi ukuaji wake uende bega kwa bega na ufundishaji, mbinu na uandaaji wa walimu wa Kiswahili.

9.0 Sera ya Elimu na Sera ya Utamaduni

Sera ya Elimu na mafunzo iliyotolewa na Wizara ya Elimu na Utamaduni mnamo mwaka 1995 inazidi kushadidia Kiingereza kuwa Lugha ya kufundishia elimu ya sekondari na vyuo vikuu kwa kutamka wazi kwamba Kiingereza kitaendelea kuwa Lugha ya Kufundishia (Educational & Training Policy 1995:45). Kwa kupitia Wizara hiyo hiyo ya Elimu na Utamaduni, serikali ilipitisha Sera ya Utamaduni mnamo mwaka 1997 kwa kuonyesha nia yake ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia angalau kwa kutamka kuwa: “Mpango maalum wa kuiwezesha elimu na mafunzo katika ngazi zote kutolewa katika lugha ya Kiswahili, utaandaliwa na kutekelezwa “ (Sera ya Utamaduni 1997:19). Katika sera hiyo, hatua ya maandalizi haikuwekwa wazi. Hata hivyo sekta ya Utamaduni ilifanya tathmini katika Mkutano wa taifa wa Sera ya Utamaduni mjini Arusha kuanzia tarehe 24-28 Mei, 1999. Mkutano huo ulibaini imani potofu kuhusiana na lugha ya kufundishia kwa kuwa watu wengi wanaamini kwamba taaluma pevu hupatikana tu kwa lugha za kigeni hususa Kiingereza. Wananchi wengi hasa wasomi hawatofautishi baina ya ufundishaji wa lugha na lugha ya kufundishia; watu wengine wanaamini kwamba kujua Kiingereza ndiko kuimarika kielimu. Aidha upungufu wa istilahi za Kiswahili, vitabu, walimu na stadi za kufundishia kwa Kiswahili ni eneo jingine lililodhihirika kuwa ni tatizo linalokwaza kutumika kwa Kiswahili.

Mikakati iliyopo kuhusu Sera ya Utamaduni ni kuwaelimisha viongozi na jamii kuhusu dhima ya lugha ya kufundishia ili kujenga imani sahihi kuhusu uwezo wa lugha ya Kiswahili kutolea elimu ya upatikanaji wa istilahi, vitabu, walimu na stadi za kufundishia (Ripoti ya Mkutano wa Taifa wa Sera ya Utamaduni 1999:40-41). Kutokana na hali hii basi, imeonekana kuwa ipo haja ya kurudisha msisimko uliokuwepo zamani kuhusu kukua kwa Kiswahili.

10.0 Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili 1995-2000

Hali ya kufifia na kulegalega kwa maendeleo ya Kiswahili iliyojitokeza imesababisha wakereketwa watafute mbinu na mikakati ya kurejesha msisimko wa kutathimini lugha uliokuwepo baada ya uhuru. Miongoni mwa mbinu hizo ni Maadhimisho ya ‘Siku ya Kiswahili’ ya kila mwaka ambayo kwa mara ya kwanza yalizinduliwa rasmi nchini Tanzania mwaka 1995 kwa madhumuni yafuatayo:

1. Kuirejesha hadhi ya Kiswahili kama lugha ya taifa na kitambulisho cha Waafrika kwa ujumla.
2. Kuwahamasisha na kuwaelimisha wananchi kuhusu masuala ya lugha na utamaduni kwa ujumla ili washiriki kwa hali na mali katika ukuzaji wa maendeleo ya Kiswahili.
3. Kuzipa msukumo juhudi za kukuza Kiswahili na fasihi yake kwa kuwatambua na kuwaenzi wale wote waliochaguliwa na wanaochangia sana katika juhudi hizo.

4. Kuwakutanisha wakuzaji na wapenzi wa Kiswahili wakiwemo watendaji wa asasi zinazokuza Kiswahili, walimu, waandishi wa vitabu, wafasiri na wachapishaji ili waweze kufahamiana na kubadilishana mawazo na kupanga mikakati ya pamoja ya kuyatekeleza majukumu hayo.
5. Kuwakutanisha wakuzaji na wapenzi wa Kiswahili kutoka katika nchi zote zinazotumia Kiswahili.
6. Kuihamasisha serikali na chama tawala kuhusu wajibu wao wa kuikuza, kuiendeleza na kuienzi lugha ya taifa.
7. Kuimarisha ufundishaji na kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kuwatambua na kuwatunuku walimu na wanafunzi bora wa somo la Kiswahili.
8. Kuanzisha mfuko wa kudumu wa kuendeleza Kiswahili na kukusanya fedha kwa ajili ya mfuko huo.

Maadhimisho ya kwanza ya siku ya Kiswahili yaliyofanyika Dar es Salaam tarehe 4/1/95 – 7/1/95 na kuzinduliwa rasmi na Rais Ali Hassan Mwinyi tarehe 7/1/95 yalikuwa na Kongamano la Siku ya Kiswahili (taz. Ripoti ya Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili 1995, BAKITA: (5-6) lililofanyika Ukumbi wa Goethe Institut). Jumla ya makala 11 zilitolewa, na tatu miongoni mwake zilikuwa:

- “Nafasi ya Kiswahili Kama Lugha ya Kufundishia Masomo ya Shahada,” Profesa Geoffrey V. Mmari.
- “Kiswahili Kama Lugha ya Kufundishia Katika Shule za Sekondari, Tanzania,” Dkt. Casmir M. Rubagumya.
- “Matumizi ya Kiswahili Katika Uwanja ya Ufundi,” A.H. Mapande.

Makala hizo zilifufua mjadala unaohusu Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Washiriki walionyesha masikitiko yao kutokana na kuchelewa kufanyika kwa uamuzi wa kukitumia Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari na elimu ya juu, na kwamba mawasiliano na serikali kuhusiana na suala hilo yaendeleo.

Katika maadhimisho yaliyofanyika Dodoma mwaka 1998, suala la Kiswahili katika elimu lilijadiliwa. Makala mbalimbali zilitolewa na kujadiliwa kuhusu elimu maalum, upataji istilahi za kisayansi na maandalizi ya Kiswahili ili kumudu fani ya hisabati (trigonometri na aljebra).

Semina hiyo, iliyoshirikisha walimu wa shule za Dodoma ilileta msisimko mkubwa na kupendekeza kwamba kuitishwe semina nyingine yenye hadhira pana zaidi kuhusu Kiswahili na Elimu.

Mwaka 2000 Januari, katika maadhimisho yaliyofanyika Dar es Salaam, mada kuu ilikuwa Kiswahili Kama Lugha ya Kufundisha Elimu ya Juu. Mada mbalimbali zilitolewa zikiwemo: “Baadhi ya Vipingamizi vya Kiutawala vya Kutumia Kiswahili Sekondari na Vyuo,” iliyotolewa na Profesa M.M. Mulokozi; “Kufundisha Sayansi kwa Kiswahili Kutaleta Tija kwa Sayansi, Kiswahili na Kiingereza,” Bw. Omari M.

Kiputiputi; “Matatizo ya Kutumia Kiingereza Kufundishia Katika Shule za Sekondari na Vyuo vya Juu Tanzania,” iliyotolewa na Dkt. M.A.S. Qorro; “Mikakati ya Utekelezaji wa Sera ya Kiswahili kwa Kufundishia,” na Dkt. Z.S. Mochiwa.

Mada zote hizo nne zilionyesha kwamba Kiswahili kina uwezo mkubwa wa kumudu kufundishia elimu ya juu hasa kutokana na matatizo yanayoyapata wanafunzi wa viwango vyote vya elimu ya juu katika kumudu masomo ya fani zote. Aidha ilidhihirika kwamba lugha ni chombo kinachotusaidia kuongoza fikra zetu na kwamba ni muhimu kutekeleza sera ya kutumia Kiswahili kufundishia ngazi zote za elimu nchini Tanzania.

Washiriki wa semina, baada ya mjadala wa kulisimua, walitoa mapendekezo mbalimbali miongoni mwayo yakiwa:

- Programu ya utekelezaji wa Sera ya Utamaduni iliyofanyika Arusha ianze kutekelezwa kwa dhati katika bajeti ya serikali ya mwaka 2000/2001. Mwaka huo uwe tarehe rasmi ya kuanza kufundisha kidato cha I kwa Kiswahili;
- Sera ya kutumia Kiswahili kufundishia shule zote za msingi izingatiwe na shule zote isipokuwa chache ambazo ni za kimataifa hasa. Serikali isimamie utekelezaji wa sera hii na iwachukulie hatua wanaoikiuka;
- Itamkwe wazi katika katiba ya nchi kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa;
- Zitungwe sheria zenye kuhimiza matumizi ya Kiswahili katika vyombo vya habari, sinema na video na mahakamani;
- Asasi za kukuza Kiswahili zitengewe bajeti maalum kutokana na bajeti ya serikali, fedha za bahati nasibu, n.k. Aidha asasi zenyewe ziwe na mikakati ya kujiongezea mapato;
- Matatizo ya mashirika ya uchapishaji vitabu yashughulikiwe kitaifa kwa mashauriano na sekta hiyo;
- Vyombo vya Kiswahili, asasi za Kiswahili na vyama vya Kiswahili viunde chombo ambacho kitaweza kuisukuma serikali ili kutekeleza sera ya kutumia Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari na vyuo;
- Ziwepo semina kwa ajili ya kuwaelimisha wabunge na viongozi kuhusu matatizo ya kufundisha kwa Kiingereza katika shule za sekondari na vyuo;
- Ziwepo kampeni za kupiga vita kasumba iliyopo katika jamii kuwa Kiswahili hakina uwezo wa kutolea elimu katika shule za sekondari na vyuo.

11.0 Kamati ya Maandalizi ya Mpango Kamambe wa Kukiwezesha Kiswahili kuwa Lugha ya Kufundishia

Kwa kutambua umuhimu wa kuchukua hatua ili kukiwezesha Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia elimu ya Sekondari na elimu ya juu, mwezi Aprili mwaka 2000, serikali iliunda kamati ya wataalamu kutoka vyombo na asasi mbalimbali zinazohusika kwa njia moja au nyingine na ukuzaji wa Kiswahili na elimu nchini ili kuandaa programu ya utekelezaji wa sera ya kutumia Kiswahili kufundishia. Kamati hiyo imepewa jukumu la kuchambua na kuchanganua mahitaji halisi ya kufanikisha azma hiyo yakiwemo: mahitaji ya walimu, mafunzo, vitabu (vya kufasiriwa na kutungwa) na tarehe rasmi ya kuanza utekelezaji. Kuwepo kwa mpango kamambe wa kukiwezesha Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia kutawezesha wafadhili kuisaidia serikali, ili kutekeleza azma hii.

Matatizo

Pamoja na vizingiti vyote vya kukua na kuenea kwa Kiswahili vilivyodhihirika hapa na pale katika makala haya, kuna tatizo jingine kubwa la msingi ambalo ni BAKITA kukosa nguvu ya kisheria ya kumtia hatiani mtu au chombo. Sheria ya BAKITA iliyopo hivi sasa ni kushauri tu kusaidia na kuunga mkono juhudi za kukuza Kiswahili nchini.

Tatizo jingine ni ukosefu wa fedha, vitendea kazi na wataalam wa kutosha. Katika takriban kipindi cha miaka 10 sasa BAKITA haijafanya warsha za usanifishaji.

Tatizo hili linasababisha usanifishaji wa istilahi uwe mgumu hasa kwa kuzingatia kwamba shughuli kama hiyo inahitaji warsha na vikao vya kuthibitisha istilahi. Haya yanadhihirishwa na jedwali la bajeti lifuatalo kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 1996/97 – 1999/2000, hali ambayo haitofautiani na miaka mitano kabla ya hapo.

Bajeti ya Bakita kwa Miaka 4

Mwaka	Maombi	Zilizotolewa
1996/97	105,249,725	44,688,405
1997/98	125,029,120	54,957,696
1998/99	160,114,188	54,023,288
1999/2000	187,111,276	573,243
Jumla	577,504,209	210,953,765
Nakisi		366,550,444

Tanbihi: Fedha zilizotolewa ni kwa ajili ya mishahara tu, ya wafanyakazi wa BAKITA.

12.0 Hitimisho

Makala haya yameonyesha juhudi zilizofanywa na BAKITA katika kukuza na kuendeleza Kiswahili kama lugha ya kufundishia na vipingamizi vilivyofisha juhudi hizo. Aidha yameonyesha kwamba kuzidi kuchelewa kufanya maamuzi ya haraka kuhusu Kiswahili kufundishia Elimu ya Juu kunadumaza elimu. Pia utoaji fedha pungufu hakutaiendeleza lugha ya Kiswahili. Mwisho mwelekeo wa kung'ang'ania Kiingereza katika elimu ya sekondari na ya juu kutazidi kuligharimu taifa fedha nyingi kwa manufaa ya asilimia ndogo ya watu na kuacha umma wa Tanzania katika lindi la umbumbumbu. Hata hivyo, tunaipongeza serikali kwa hatua ya Aprili, 2000 ya kuteua Kamati ya Maandalizi ya mpango kamambe wa kukiwezesha Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia, ikiwa ni sehemu ya mpango wa maendeleo ya sekta ya utamaduni.

Marejeo

BAKITA (1970), "Taarifa ya Semina ya Kiswahili," iliyofanyika Tarehe 5-9 Juni, 1970.

BAKITA (1995), "Ripoti ya Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili ya Mwaka 1995."

Campell na Qorro 1986, *A Survey of the Reading Competence in English of Secondary School Students in Tanzania*. DUP. Dar es Salaam.

Criper, C. na Dodd, W., (1984), 'Report on the Teaching of English Language and its Uses as Medium of Instruction in Tanzania', Dar es Salaam. The British Council.

Msanjila Y.R. (1990), "Problems of Teaching Through the Medium of Kiswahili in Teacher Training Colleges in Tanzania". *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, II/4:307-318.

Mlama, P. na Materu, M. (1980) "Haja ya Kutumia Kiswahili kama Lugha ya Kufundishia Katika Elimu ya Juu", *Lugha Yetu* 35 na 36, Dar es Salaam, BAKITA.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1982), "Mfumo wa Elimu ya Tanzania 1981 – 2000," *Ripoti ya Mapendekezo ya Tume ya Rais ya Elimu*, Juzuu I – Dar es Salaam.

Qorro, M. (1996) "Matumizi ya Kiswahili, Kiingereza Kufundishia: Wanaotoa maoni. Hawajafanya Utafiti". *Rai*, Desemba 5-11, 1996.

Wizara ya Elimu ya Utamaduni (1995), "Education and Training Policy," Dar es Salaam.

Wizara ya Elimu na Utamaduni (1997), "Sera ya Utamaduni," Dar es Salaam.

Wizara ya Elimu na Utamaduni (1999) "Ripoti ya Mkutano wa Taifa wa Sera ya Utamaduni," uliofanyika Arusha tarehe 24/02/1999.